

Wapendwa Jumuiya ya Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb,

Ni kwa moyo mzito ninazungumza nanyi leo tunapokuwa tukiomboleza msiba wa kumpoteza mwanafunzi mchanga mwerevu kutoka Shule ya Upili ya Lithonia. Vurugu isiyo na maana ambayo inaendelea kukumba jumuiya zetu ni hali ya dharura ambayo inahitaji tahadhari na hatua zetu za haraka. Hatuwezi kuruhusu macho yetu kufumba tena; wakati wa mabadiliko ni sasa.

Sauti ya jumuiya yetu ina nguvu kubwa katika kuleta mabadiliko ya kimfumo, na ni lazima tugundue hii na tuitumie ipasavyo. Tunapaswa kuja pamoja, tukiungana katika Kaunti ya DeKalb, na tutangeze kwa sauti moja kubwa kwamba imetosha. Lazima tuokoe jumuiya zetu kutoka kwenye mtego wa vurugu na tuzifanye mahali salama kwa watoto wetu.

Tuweke kando mifarakano ya siasa na tuzingatie kile ambacho ni muhimu zaidi: usalama na maslahi ya watoto wetu. Ni lazima tuondokane na watu wenye kujivuna ambao hutafuta kuzuia maendeleo, ndani na nje. Tunapaswa kutanguliza masilahi ya umma zaidi kuliko ajenda za kibinagsi, tukifanya kazi kwa kushirikiana kuelekea lengo moja.

Ili kufanikisha hii, ni muhimu kwamba tuwe na wafanyakazi wa kutosha katika shule zetu na ofisi kuu, ili kuhakikisha kwamba tuna rasilimali na msaada muhimu wa kukidhi mahitaji ya kila mtoto kila siku. Hakuna mtoto anayepaswa kukabiliwa na tishio la vurugu anapokuwa akitafuta elimu. Ni lazima tufanye mengi zaidi, tufanye chochote kinachohitajika kuwalinda na kuwalea wanafunzi wetu.

Hata hivyo, tunapaswa pia kushiriki katika kutafakari binafsi. Tunatakiwa kujitazama kwenye kioo na kuijuliza tumefanya nini au hatujafanya nini kuchangia utamaduni wa kutojali unaoendeleza mauaji haya yasiyo na maana. Hatuwezi kuendelea kutupilia mbali masuala haya kama tatizo la mtu mwingine.

Jukumu letu la pamoja ni kuunda mazingira salama kwa watoto wetu, na huanza na kila mmoja wetu. Tuungane pamoja, tutafakari kuhusu matendo yetu ya awali, tuungane kwa kusudi moja, na tukue kama jumuiya. Ni kupitia juhudhi zetu za pamoja tu ndio tunaweza kukomesha mzunguko huu wa vurugu. Watoto wetu wanastahili maisha bora zaidi, na tunawajibika kwao kuunda mustakabali mzuri na salama zaidi.

Kwa kumalizia, nawaacha na nukuu ambayo inaelezea kiini cha dhamira yetu: “*Kutafakari, kuunganisha, na kukua, yote kwa manufaa ya wote.*” Tusimame kwa umoja, bega kwa bega, na tufanye kazi kuelekea siku zijazo ambapo watoto wetu wanaweza kustawi bila woga.

Kwa pamoja tunaweza kuleta mabadiliko,

Dkt. Devon Q. Horton, *Msimamizi*

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb